

ATHARI ZA BIDHAA BANDIA

UTANGULIZI

Bidhaa bandia (feki) ni bidhaa zilizotengenezwa kwa kuiga bidhaa nyingine kwa nia ya kudanganya au kutapeli.

Bidhaa bandia zina alama za kudanganya au zinaweza kuwa na alama halisi za bidhaa au maelezo sahihi ya bidhaa lakini wahusika hawana ruhusa ya kutumia alama hizo kutoka kwa watu; mashirika au kampuni zenye hakimiliki ya alama hizo au maelezo hayo ya bidhaa.

Kulingana na sheria ya Alama ya Bidhaa ya mwaka 1963, kujishughulisha na bidhaa bandia ni kosa la jinai na linaadhibiwa kwa kifungo cha miaka 4-15 jela. Pia mkosaji anaweza kutozwa faini ya Shilingi Milioni 10-50 na bidhaa kuharibiwa kwa gharama ya aliyekamatwa nazo.

Ukubwa wa Tatizo la Bidhaa Bandia

Biashara ya bidhaa bandia inakadiriwa kuwa ni wastani wa asilimia 5-7 ya biashara yote ulimwenguni, ambayo kwa mujibu wa taarifa za mashirika mbalimbali ya kimataifa, inakadiriwa kuwa ni kati ya Dola za Marekani 250 na 600 Bilioni kwa mwaka.

Kwa Afrika Mashariki, inakisiwa kuwa thamani ya bidhaa bandia zinazouzwa katika eneo hilo ni Dola za Marekani Milioni 500 na zinakadiriwa kuwa ni asilimia 30 ya biashara yote inayofanyika katika eneo hilo.

Nchini Tanzania, tatizo la bidhaa bandia siyo suala la siku nyingi. Lilianza kujitokeza kama miaka thelathini (30) iliyopita baada ya kulegeza masharti ya biashara na kukosa mfumo wa kusimamia mwendendo wa uchumi wa soko ulipoanza kutumiaka mwaka 1986.

Biashara ya bidhaa bandia imeshamiri zaidi katika: Vifaa vya Ujenzi, Vifaa vya Umeme, Vifaa vya Elektroniki, Madawa, Betri, Viberiti, dawa za viatu, dawa za meno na dawa za binadamu. Katika baadhi ya maeneo, mathalan biashara ya vifaa vya umeme, inakisiwa kuwa asilimia 30 hadi 40 ya vifaa vyote vinavyoingizwa nchini ni bandia.

SHERIA YA ALAMA ZA BIDHAA YA MWAKA 1963

Sheria inayokataza bidhaa bandia nchini Tanzania ni sheria ya Alama za Bidhaa (The Merchandise Marks Act ; 1963 CAP 85 RE 2002) kama ilivyorekebisha mwaka 2005 na 2007 ambayo inataja kuwa kushughulika na bidhaa bandia ni kosa la jinai. Sheria ya Alama ya Bidhaa (1963) ilianza kutumika tarehe 15 Aprili 2005 miaka 42 baada ya kutungwa na kupitishwa kuwa Sheria.

MADHARA YA BIDHAA BANDIA KATIKA UCHUMI NA JAMII

Bidhaa bandia zina madhara makubwa ya moja kwa moja (harmful) kwa umma na pia zina athari kwenye uchumi wa nchi. Madhara ya bidhaa bandia katika uchumi ni kama yafuatayo:-

1. Watu wanaojishughulisha na bidhaa bandia ni wahalifu kwa hiyo mara nyingi hawalipi kodi za Serikali kama sheria inavyoagiza na endapo ikitokea wakalipa, kiasi wanacholipa ni kidogo sana na hakilingani na stahili yao kwa vile hawatangazi thamani halisi ya bidhaa zao;
2. Mtengenezaji bidhaa bandia hawajibiki kwa dhati na athari zinazoweza kumsibu mlaji maana hajitambulishi kuwa yeye ndiye mtengenezaji wa bidhaa hizo;
3. Wakati mwingine Wafanyabiashara wa bidhaa bandia huuza bidhaa zao kwa walaji kwa bei karibu sawa na bei ya bidhaa halisi hivyo kuwadanganya na kuwaibia walaji;
4. Kwa ujumla wake bidhaa bandia ni bidhaa duni (sub-standard) na bidhaa za aina hii zina madhara makubwa kwa mtumiaji. Iwapo bidhaa hizo ni vyakula na madawa, zinaweza kusababisha vifo kwa watu na kwa bidhaa bandia za vifaa vya umeme na vya ujenzi matokeo yake ni uharibifu mkubwa wa mali na makazi;
5. Bidhaa bandia zinamwondoa kwenye soko mfanyabiashara wa bidhaa halisi kwa vile mfanyabiashara huyu hawezi kuuza bidhaa zake zikishindana na bidhaa bandia zinazofanana na bidhaa zake halisi kwa sababu zile bandia huuzwa kwa bei ya chini;
6. Kukithiri kwa bidhaa bandia kunawaogopesha na kuwatorosha wawekezaji wapya na wale ambao tayari wapo nchini katika shughuli za kiuchumi wanaweza kulazimika kufunga shughuli zao na hivyo kulikosesha taifa mapato na rasilimali na upotevu wa ajira kwa wananchi;
7. Mwisho, mlaji anayenunua bidhaa bandia huishia kutumia fedha nyingi zaidi kwa bidhaa ile ile kuliko kama angenunua bidhaa halisi kwa vile bidhaa bandia muda wake wa kuishi ni mfupi na hivyo humlazimisha mlaji kurudia kununua bidhaa hiyo mara nyingi zaidi.

Ili kuepokana na madhara hayo ambayo muathirika zaidi ni mlaji wa mwisho, wananchi wanahimizwa kuchunguza bidhaa kwa makini kabla ya kuzitumia, ili kubaini udanganyifu unaoweza kufanywa katika bidhaa husika.

DHANA POTOFU KUHUSU BIDHAA BANDIA

Kumekuwa na mitizamo na dhana mbalimbali potofu kuhusu bidhaa bandia. Mitazamo hii imeendelea kuwafanya watu mbalimbali kuwa wahanga wa bidhaa bandia na kujikuta

wakiendelea kuzitumia na kuathiriwa nazo badala ya kuziepuka. Mitazamo na dhana hizo ni pamoja na hizi zifuatazo:

Bidhaa bandia na Bidhaa Duni kufananishwa:

Bidhaa inakuwa duni inapokuwa haikidhi kiwango kilichowekwa kitaifa au kimataifa na mashirika ya kudhibiti viwango vya ubora kwa ajili ya matumizi salama ya bidhaa hiyo.

Bidhaa bandia siyo lazima iwe bidhaa duni, inaweza kuwa bidhaa nzuri lakini kuna tatizo zito la kisheria kuhusiana na bidhaa ya namna hiyo kuwa imetumia hataza (nembo/alama ya biashara) bila ruhusa ya mmiliki wake, jambo ambalo ni wizi na kosa la jinai.

Bidhaa Bandia kuwasaidia watu wa kipato cha chini

Si kweli kuwa bidhaa bandia zinamsaidia mlaji kwa kigezo cha bei ndogo pekee. Bidhaa bandia zina maisha mafupi hivyo mnunujaji hujikuta akirudia rudia kununua bidhaa ile ile kwa muda mfupi na hivyo kuwa gharama kubwa mwisho wa mwaka. Ukweli ni kwamba, kwa kuwa watengenezaji wa bidhaa bandia hawapendi kufahamika, ni dhahiri kuwa hawataki kuwajibika kwa tatizo lolote litakalojitokeza baada ya mauzo ya bidhaa hizo.

Bidhaa bandia na Ugunduzi

Kumekuwepo dhana kuwa mapambano ya kuzuia bidhaa bandia yanaweza kuwa yanadumaza ugunduzi mpya na teknolojia. Sheria ya Alama za Bidhaa haizuii maendeleo ya teknolojia yanayoleta ugunduzi mpya wa bidhaa, bali sheria inazuia watu kutumia nembo au alama ya bidhaa ya mtu mwingine bila idhini yake.

Mara nyingi tumeona watu au makampuni yakiiga teknolojia ya watu wengine katika kutengeneza bidhaa (reverse engineering) na hili siyo kosa. Kosa ni kutumia nembo au alama inayoitambulisha bidhaa ambayo siyo yako ili kufanyia biashara yako.

Kwa Maelezo Zaidi Wasiliana na:

Mkurugenzi Mkuu
Tume ya Ushindani, Ghor 2,
Jengo la GEPF House
Kitalu Na. 37 Regent Estate
Barabara ya Bagamoyo
S. L. P 7883
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2926128-31
Faksi: +255 22 29626126

Barua pepe: info@competition.or.tz
Tovuti: www.competition.or.tz